TANGAZO LA SERIKALI Na. 816 la tarehe. 20/9/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16 (1))*

SHERIA NDOGO YA UTAMADUNI NA VIBALI VYA BURUDANI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Utamaduni na Vibali vya Burudani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"utamaduni" maana yake ni ngoma za asili, disko, maigizo, mazingaombwe, sinema, michezo na tiba za kienyeji;

"michezo" maana yake ni mazoezi ya mwili yaliyodhibitiwa na ya ushindani mfano michezo ya mpira, kuogelea, riadha, bao, drafti na sarakasi; na

"sanaa" maana yake ni uzuri uliojiepusha katika umbo

lililosanifiwa mfano maigizo, mazungumzo, semi, ngoma, shairi na maonesho.

Vibali na eneo

4.-(1) Mtu yeyote anayekusudia kuendesha shughuli za kiutamaduni katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuwa na kibali.

(2) Maombi ya kibali cha kuendesha shughuli za kiutamaduni yatawasilishwa Halmashauri kwa maandishi.

(3) Maombi ya kibali cha kuendesha shughuli za tiba za kienyeji yatawasilishwa Halmashauri kwa maandishi yakiambatishwa barua kutoka Serikali ya Kijiji na Mganga Mkuu wa Wilaya ambaye atathibitisha uwezo wa mwombaji katika tiba za asili.

(4) Maombi kwa ajili ya kupiga ngoma za tambiko, harusi na tiba za kienyeji yatawasilishwa Halmashauri kwa maandishi yakiambatishwa na barua kutoka Serikali ya Kijiji anachoishi mwombaji.

Vikundi

5.-(1) Vikundi vyote vinavyoendesha shughuli za sanaa na muziki katika eneo la Halmashauri vitatakiwa kusajiliwa na kupewa hati ya usajili na Halmashauri.

(2) Maombi ya usajili wa vikundi vya utamaduni yatawasilishwa kwa kujaza fomu itakayotolewa na Halmashauri.

Kibali

6.-(1) Kibali kilichotolewa na Halmashauri hakitatumiwa na mtu mwingine.

(2) Kila mwenye kibali atalazimika kuonyesha kibali wakati wowote atakapotakiwa kufanya hivyo na Afisa Mwidhiniwa.

Ada ya vibali

7. Kutakuwa na ada ya vibali itakayolipiwa Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza:

Isipokuwa kwamba, vikundi vya utamaduni vinavyoendeshwa na Serikali au Halmashauri havitatozwa ada yoyote katika kuendesha shughuli hizo.

Adhabu

8. Mtu anayekiuka masharti ya kifungu chochote cha Sheria Ndogo hii anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki

mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufililisha kosa

9. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa

## JEDWALI LA KWANZA

(*Limetengenezwa chini ya kifungu cha 7)*

### ADA YA VIBALI

| | | | Ada kwa siku Tshs | Ada kwa mwaka Tshs |
|---|---|---|---|---|
| **(a)** | Ada ya kusajili kikundi cha sanaa na muziki | | | 30,000/= |
| **(b)** | Kibali cha disko kwa siku moja:- | | | |
| | (i) | Kikundi cha ndani ya Wilaya | 12,000/= | |
| | (ii) | Kikundi cha nje ya Wilaya lakini ndani ya Mkoa | 30,000/= | |
| | (iii) | Kikundi toka nje ya Mkoa 10% ya mapato lakini si chini ya shilingi | 30,000/= | |
| **(c)** | Kibali cha kupiga dansi siku moja :- | | | |
| | (i) | Kikundi cha ndani ya Wilaya | 20,000/= | |
| | (ii) | Kikundi toka nje ya Wilaya lakini ndani ya Mkoa | 30,000/= | |
| | (iii) | Kikundi toka nje ya Mkoa 10% ya mapato lakini si chini ya shilingi | 50,000/= | |
| **(d)** | Kibali cha kuonyesha sanaa za maonyesho (sinema, video, maigizo, kumbi za mpira, sarakasi, ngumi, ngoma, kunyanyua vyuma na kadhalika) | | | |
| | (i) | Sanaa za maonyesho ngoma, maigizo, sarakasi, ngumi na kadhalika kwa siku moja | 10,000/= | |
| | (ii) | Sinema au video kibali | 10,000/= | |
| | (iii) | Ada ya video au sinema | | 40,000/= |
| | (iv) | Kikundi cha ndani ya Wilaya | 20,000/= | |

*Tangazo la Serikali Na.816 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| (v) | Kikundi toka nje ya Wilaya lakini ndani ya mkoa | 30,000/= |
| (vi) | Kikundi nje ya Mkoa 10% ya mapato lakini si chini ya Shilingi | 30,000/= |

**(e)** Kibali cha kuuza dawa za asili 20,000/=

**(f)** Kibali cha kuendesha tiba ya asili ndani ya eneo la Halmashauri

| | | |
|---|---|---|
| (i) | Waganga toka nje ya Wilaya | 30,000/= |
| (ii) | Waganga maarufu ndani ya Wilaya | 30,000/= |
| (iii) | Waganga wadogo ndani ya Wilaya | 30,000/= |

(g) Ada kwa ajili ya kuzuru sehemu za makumbusho au za kihistoria kwa mtu mmoja

| Mhusika | Raia (Tshs) | Asiye Raia (Us $) |
|---|---|---|
| Mtu mzima | 2000/= | 5/= |
| Mwanafunzi | bure | 3/= |

**(h)** Ada kwa ajili ya kumbi za Starehe au maeneo ya miji kwa ajili ya shughuli za maonyesho, starehe (Social clubs and Halls) viwanja vya michezo (Stadium) ambazo hutumika kwa kutoza viingilio kwa kila mwaka ni kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| (i) | Kumbi za kuonyesha mpira | 30,000/= |
| (ii) | Kibali cha kuendesha kumbi za sherehe | 30,000/= |

(i) Kibali cha kunasa nyimbo za asili, upigaji picha vitu na vikundi vyenye kujishughulisha na fani za kiutamaduni kwa mara moja

| Raia (Tshs) | Asiye Raia (Us $) |
|---|---|
| 5000/= | 5$ |

| | | |
|---|---|---|
| **(j)** | Kibali cha kuendesha fete kwa siku moja | 20,000/= |
| **(k)** | Kibali cha kuchezesha michezo ya mpira wa miguu kwa kutoza viingilio kwenye viwanja vya michezo (Stadium) kokote kule ndani ya eneo la Halmashauri ya Wilaya itakuwa | 20,000/= |

**(l)** Kibali cha kuendesha shughuli zozote za mikutano ya kidini nje ya maeneo ya makanisa au misikiti bure (lakini lazima kibali kitolewe).

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 9)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFILILISHA KOSA

Mimi …………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ……………………………………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Kalambo, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha …… cha Sheria Ndogo ya Utamaduni na Vibali vya Burudani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ya mwaka, 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya mwezi…………..… mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

Mbele yangu :

Jina: …………………………………..……………………

Saini……………………….………………………..………

Wadhifa: ………………………………………………………

Tarehe……………………………………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo uliofanyika tarehe 4/11/2022 na kushuhudiwa lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

SHAFI K. MPENDA,
*Mkurugenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Kalambo*

DAUDI NZELANI SECHOME,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Kalambo*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
19 Julai, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB.)
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*,